



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUTOA HUDUMA ZA KUKODISHA MAGARI KWA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA. 10006827

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kutoa huduma ya kukodisha magari kwa ajili ya matumizi ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Katika upande wa Tanzania bomba litapita katika mikoa nane (8), halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Maelezo mafupi ya huduma yanahusiana na utoaji wa huduma ya kukodisha magari ikiwa ni pamoja na huduma ya matengenezo ya gari mahususi kwa ofisi kuu iliyoopo Dar es Salaam na uwandani katika mikoa nane (8) ambamo bomba la mafuta litapita nchini Tanzania.

Huduma itajumuisha:

- Utoaji wa Huduma ya Kukodisha Magari.
- Utoaji wa huduma za matengenezo ya

kuhakikisha usalama wa magari na matengenezo ya muda maalum.

- Huduma zinazohusiana na usimamizi wa matairi na marekebisho/matengenezo yake.
- Huduma zote tajwa pamoja na kuwasilisha orodha ya watendaji waliofuzu pia na huduma ya marekebisho ya magari madogo na huduma nyingine zinazohusiana na magari.

VIGEZO MUHIMU:

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa Kampuni ya kukodisha magari kulingana na sheria za Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Leseni ya biashara.
- Orodha ya matawi nchini Tanzania.
- Maelezo kwa ufupi ya uzoefu wa utoaji huduma ya kukodisha magari na kutoa huduma ya matengenezo ya magari.
- Watendaji wanaopendekezwa kwa ajili ya kufanya kazi katika huu Mradi na uzoefu wao katika kutoa huduma kama inayohitajika.
- Uthibitisho wa usajili katika Kanzi Data ya Watoto Huduma wa Ndani (LSSP) ya EWURA wakati wa kuwasilisha taarifa ya nia unahitajika.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe:

tala.mufti@external.total.com (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 14 Juni 2021.

Nyahur: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).